# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS-TAMISEMI.

**NAMBA ZA SIMU:**
**MKUU WA SHULE: 0763209820/0628309328**
**MAKAMU MKUU WA SHULE: 0763 751907/0622544092**
**MTAALUMA: 0689567779 / 0712603089/0621731367**

**SHULE YA SEKONDARI BUTUNDWE,**
**S.L.P 442,**
**GEITA.**
**19/04/2024.**

**MZAZI /MLEZI WA MWANAFUNZI:................................................................**

**S.L.P........................**

**................................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUTUNDWE HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA VIJIJINI MKOA WA GEITA MWAKA 2024**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2024 Tahasusi ya **CBA** shule ya sekondari Butundwe ipo umbali wa kilometa 42 magharibi mwa mji wa Geita na kilometa 15 kutoka mji mdogo wa Katoro. Usafiri wa Hiace/Basi kutoka mjini Geita unapatikana katika kituo cha Mabasi Mjini nauli ni shilingi 5000/= kwa watakao shukia mji mdogo wa Katoro usafiri wa Gari unapatika kwa nauli ya Sh. 4000/=.
   Muhula wa masomo unaanza tarehe 01/07/2024. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe iliyoelekezwa na OR-TAMISEMI. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …../07/2024 kama ilivyoelekezwa na OR-TAMISEMI.
2. Mambo muhimu ya kuzingatia:

   **A. BIMA YA AFYA.**

   Kila mwanafunzi aje na kadi ya Bima ya Afya.Kwa mwanafunzi amabaye hana bima ya afya lazima aje na Namba ya NIDA pamoja shilingi 50,400/= kwa ajili ya kusajiliwa NHIF kwa mwaka (pesa hii isilipwe Benki, Mzazi/Mlezi aje nayo wakati wa kuripoti). Shule haitagharamia matibabu ya mwanafunzi mgonjwa asiye na BIMA kwa uzembe wake mwenyewe.Hivyo ni lazima kila mwanafunzi kuwa na BIMA.

   B. **SARE YA SHULE**.

   (a) Mashati mawili (02) meupe ya Tetron yenye mikono mirefu.
   (b) Sketi mbili (02) moja rangi ya dhahabu (Pure Gold) amabayo itavaliwa Jumatatu hadi Jumatano, ya pili rangi ya purple Pink itavaliwa siku za Alhamisi na Ijumaa. zenye marinda

mapana na ndefu inayogusa kifundo cha mguu, mkanda nchi mbili (02) (mama Samia Type)vitambaa viwe halisi(Original) mwanafunzi mwenye sketi fupi hatapokelewa.

(c) Kwa wale wa dhehebu la Kiislamu mwanafanzi awe na Ijabu nyeupe.

(d) Tai mbili(2) Moja rangi ya dhahabu(Gold) nay a pili rangi ya purple pink zenye mistari ya mshazali.

(e) Masweta rangi ya ugoro (Nzito original)

(f) Viatu vyeusi vya ngozi (kisigino butu) vya kufunga na kamba.
NB: Mwanafunzi mwenye viatu tofauti (simple) hatapokelewa.

**C. VIFAA VINGINE MUHIMU.**

(g) Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (02) au zaidi.

(h) Tshirt aina ya Sport Origanal yenye kora rangi ya creem.

(i) Tracksuit ya rangi ya pink kwa ajili ya michezo.

(j) Tracksuit ya rangi ya bluu kwa ajili ya kusomea usiku (preparation).

(k) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo.

(l) Shamba dress- gauni rangi ya kijani giza kitambaa kizito.Mshono wa solo,urefu iguse kifundo cha mguu.

(m) Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele au kuweka dawa kwenye nywele. Pia vipodozi na manukato hayaruhusiwi.

**NB:Ili kuepuka usumbufu wa kukosea rangi na mishono na kuleta kadhia kwa mzazi mahitaji yafuatayo mzazi anaweza kuyapata karibu na maeneo ya shuleni:**
**Skirt, tai, T-shirt, sweta na tracksuit aina zote mbili pamoja shamba dress.**

D. **MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJA NAYO**.

**(a) VIFAA VYA MASOMO:**

i. Daftari kubwa 10 (counter books) ( quire 3 au 4).
ii. Kalamu za kutosha.
iii. RIM Mbili (2) za karatasi A4 .
iv. Vitabu vya masomo kulingana na tahasusi uliyochaguliwa (orodha imeambatanishwa)
v. Faili moja (folder file)
vi. Scientific calculator.
vii. Dissection kit.

**E. VIFAA VINGINE MUHIMU.**

i. Mfagio wa nje (chelewa mrefu uliofungwa mti) mmoja.
ii. Mfagio wa ndani (soft broom) mmoja.
iii. Ndoo moja ya LITA 20 kwa ajili ya matumizi shule na ndoo moja LITA 10 kwa matumizi binafsi ya kufulia/kuogea.
iv. Squeezer ( mfagio wa kukaushia maji)
v. Jembe lenye mpini.
vi. Fyekeo moja na reki moja.

**F. VIFAA VYA BWENI.**

i. Godoro jipya futi 2.5x6 aina ya Confy au Super Banko.

ii. Shuka mbili moja rangi ya bluu bahari nay a pili rangi nyeupe.
iii. Foronya mbili za bluu bahari na mto wake na nyeupe na mto wake.
iv. Blanketi moja.
v. Neti moja futi 4 rangi nyeupe pembe nne.
vi. Sanduku la chuma (tranker) na kufuli lake.
vii. Nguo ya kulalia (night dress).
viii. Taulo, kitenge/kanga (jozi moja), kanda mbili, sabuni za kutosha, miswaki, dawa ya meno kubwa, soap dish, vibanio vya kuanikia nguo.
ix. Lita mbili dawa ya kufanyia usafi wa choo.
x. Taa ya solar kwa dharura.(Ni lazima)
xi. Vyombo vya chakula kama vile sahani, kijiko, kikombe, bakuli na chombo cha kutunzia
xii. maji ya kunywa.
xiii. Viatu vya wazi (open shoes) jozi mbili.

NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na suruali na pedo na nguo nyingine zinazofanana na hizo. Nguo za nyumbani hazina nafasi shuleni.

Wakati wa kuripoti mwanafunzi aje akiwa amevaa sare ya shule.

**G. MICHANGO YA SHULE.**

Mwanafunzi wa bweni atalipa michango ya shule, Benki nambari **NMB 31001100556 JINA LA AKAUNTI NI BUTUNDWE SECONDARY SCHOOL RECURENT ACCOUNT.** Tafadhali, hakikisha unaandika jina la mwanafunzi husika wakati wa kufanya malipo. Mwanafunzi aje na hati ya malipo ya Benki (pay in slip) siku ya kuripoti shuleni. Aidha, mchango wa nembo na kitambulisho vitalipwa moja kwa moja shuleni siku ya kuripoti.

Michango inayotakiwa kulipwa na kila mwanafunzi ni kama ifuatavyo:

| **Na.** | **AINA YA MCHANGO** | **KIASI** |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80000/=** |

- Fedha hizo zilipwe katika akaunti ya benki iliyotajwa hapo juu isipokuwa fedha za kitambulisho na nembo ambazo zitalipwa taslimu mzazi aje nazo mkononi.

**3:0 Sheria na kanuni muhimu za shule.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3:1 Sheria na kanuni za shule.**

(i). Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(ii). Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
(iii). Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku(Night preparation)
(iv). Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
(v). Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(vi). Kutunzi usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(vii). Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(viii). Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(ix). Kutunza mali za shule.
(x). Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari na
(xi). Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwanafunzi mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumiwa na mwanafunzi mmoja tu.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa shule.( Msiba au Ugonjwa)**

### 3:2. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i). Wizi.
(ii). Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa.
(iii). Kugoma na kuhamasisha migomo shuleni.
(iv). Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
(v). Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
(vi). Uvutaji wa sigara na madawa ya kulevya kwa ujumla.
(vii). Uasherati, mapenzi ya jinsia moja na kuolewa.
(viii). Kupata ujauzito au kutoa mimba.
(ix). Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(x). Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xi). Kumiliki na kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xii). Kudharau bendera na wimbo wa Taifa.
(xiii). Kufanya jaribio lolote la kujidhuru au kujiua.
(xiv). Uhaaribifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu muhimu.**

(i). Fomu ya Uchunguzi wa afya(Medica Examination Fomu)ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.

(ii). Nakala ya matokeo ya kidato cha nne( Result slip)

(iii). Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iv). Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule na;

(v). Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za simu.

Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Nakutakia maandalizi mema.

**KARIBU SANA BUTUNDWE SEKONDARI.**

**MWL. HAPPINESS ADONIAS MANYAMA**

**(MKUU WA SHULE)**

# GEITA DISTRICT COUNCIL

## BUTUNDWE SECONDARY SCHOOL P. O. BOX. 442, GEITA.

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical officer in respect of Butundwe secondary school.

1. Full name of student………………………………………………………………………………..
2. Sex …………………………………………………………………………………………………
3. HGB test……………………………………………………………………………………………
4. Stool ……………………………………………………………………………………………….
5. Urine ……………………………………………………………………………………………..
6. TB test……………………………………………………………………………………………..
7. Eye Examination………………………………………………………………………………..
8. Chest ……………………………………………………………………………………………..
9. Abdomen…………………………………………………………………………………………..

**ADDITIONAL INFORMATION.**

Physical defects or impairments, infections, cronic or heredity (family disease)…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………….

I certify that I examined the above student and considered that; He/She is physically or not physically fit for further studies.

**Name:………………………………………………………………………Signature………………………**

**Date………………………………………Official Stamp……………………………………………..**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA

**SHULE YA SEKONDARI BUTUNDWE, S. L. P 442, GEITA**

**FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE**

**(ijazwe kwa herufi kubwa na irudishwe kwa Mkuu wa Shule)**

1.0 Jina la mwanafunzi……………………………………………Tarehe ya kuzaliwa…………..
Wilaya………………Mkoa…………......Taifa…………………………

- 1.1 Shule ya sekondari unayotoka………………………………………………..
- 1.2 Jina la Mzazi/Mlezi (wa kiume)……………………………………………….
- 1.3 Namba ya simu………………………………………………………………
- 1.4 Kazi ya Mzazi/ Mlezi…………………………………………………………
- 1.5 Jina la Mzazi/ Mlezi wa kike…………………………………………….
- 1.6 Namba ya simu……………………………………………………………….
- 1.7 Anuani yake……………………………………………………………………
- 1.8 Kazi ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………………..
- 1.9 Jina na anuani ya jamaa/ ndugu anayeishi karibu na shule hii (kama yupo)………………………………………………………………………………….

## 2.0 AHADI ZA MWANAFUNZI

(a) Mimi…………………………………………nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote ambayo ni pamoja na sheria na kanuni za shule na nimekubali/sikubali kujiunga kidato cha tano katika shule ya sekondari Butundwe.

(b) Kwahiyo, naahidi kwamba nitatimiza sheria zote za shule nakutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa. Sitashiriki katika vitendo vya kuhujnumu wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**…………………………………………………………………………..**

**Tarehe na saini ya Mwanafunzi.**

## 3.0 AHADI ZA MZAZI/MLEZI

(a) Mimi ……………………………………………..Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi…………………………………………………………………nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule na walimu kwa ujumla katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa atzitii sheria zote za shule na kuyatimiza mabo yote yaliyotajwa.

(b) Nitafanya kila niwezalo kumuwezesha mwanangu kufika shuleni siku ya shule bila kuchelewa ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa ya maandishi pale mwanafunzi anapokuwa na tatizo la kumfanya asihudhurie masomo.

**…………………………………………………………………………..**

**Tarehe na saini ya mzazi/mlezi.**

**NB.**Mzazi/ndugu ambaye picha yake haipo kwenye fomu hii haruhusiwi kuja kumwona mwanafunzi.

| PICHA NAMBA 1 | PICHA NAMBA 2 | PICHA NAMBA 3 | PICHA NAMBA 4 |
|---|---|---|---|
| | | | |

**RANGI ZA SARE ZA SHULE ZA MWANAFUNZI.**

Siketi rangi ya dhahabu



Track suit rangi ya Pinki



Track suit rangi ya Blue



Shati jeupe mikono mirefu



Sketi ya PINK PURPLE



Mfano wa Tai



**4:1.HESHIMA**

Wanafunzi wote wanatakiwa:

(i). Kutii kengele.

(ii). Kuvaa sare ya shule kwa unadhifu na kwa kufuata ratiba ya uvaaji wa sare hiyo.

(iii). Kusimama kwa unadhifu na ukakamavu wakati wa paredi.

(iv). Kusimama na kusalimia wafanyakazi wote na wageni.

(v). Wasitoke darasani bila ruhusa.

(vi). Wasipige kelele madarasani na mabwenini.

(vii). Waheshimiane wao kwa wao na wawaheshimu viongozi wao.

(viii). Kuwaheshimu watu wote waliopo shuleni pamoja na maeneo ya jirani yanayozunguka shule na nje ya shule.

**Mwanafunzi atakayekiuka kifungu 4.1 (i) hadi (vii) atakuwa ametenda kosa. Adhabu kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.**

**4:2. MAVAZI**

Mwanafunzi anatakiwa avae sare ya shule kulingana na ratiba ya siku. Mwanafunzi haruhusiwi:

(i). Kuvaa kofia, viatu vya ghorofa ( high heels ) au/ na mapambo mengine yoyote.

(ii). Kuwa na nywele ndefu.

(iii). Kusuka nywele au kunyoa mitindo(style) ikiwemo kipara.

(iv). Kufuga kucha ndefu za mikono na miguu au kupaka kucha rangi.

**Mwanafunzi yeyote atakayetenda jambo tajwa katika kifungu 4.2 (i) hadi (vi), atakuwa ametenda kosa. Adhabu kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.**

**NB: Mwanafunzi atakayevaa mavazi yasiyo rasmi (Sare) yasioidhinishwa atanyang'anywa na hayatarejeshwa kwake**

**4:3. UTUNZAJI MALI**

Wanafunzi wote wanatakiwa

(i). Kutunza mali na vyombo vya shule kama vile vitabu, madawati, meza, viti na majengo kwa ujumla. Ni marufuku kuandika chochote katika mali hizo.

(ii). Kutunza mali zao wenyewe na zile walizokabidhiwa kwa matumizi yao wawapo shuleni.

(iii). Kurejesha vifaa vyote vya shule kama vitabu na vingine kila wakati shule inapofungwa kwa mapumziko.

(iv). Kutohamisha kifaa chochote kutoka mahali pake bila idhini. Endapo samani itahamishwa kwenye vyumba vya madarasa kwa ajili ya kujisomea/shughuli yoyote zirejeshwe kwenye vyumba husika bila kuchanganywa kuepuka usumbufu na uharibifu.

**Mwanafunzi yeyote atakayeshindwa kutimiza jambo lolote katika kifungu 4:3. (i) hadi (iv) atakuwa ametenda kosa. Adhabu kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo.**

**NB: MWANAFUNZI ATAKAYESABABISHA UPOTEVU AU UHARIBIFU WA MALI YA SHULE ATALIPA MALI ALIYOPOTEZA/ALIYOHARIBU KWA GHARAMA HALISI YA MALI HIYO.**

**4:4. CHAKULA**

Chakula Cha wanafunzi kitapatikana shuleni. Hakutakuwa na chakula maalumu. Wanafunzi wote watakula chakula kilichoidhinishwa shuleni.Mwanafunzi haruhusiwi kubeba au kuagiza chakula kutoka nje ya shule.

**Atakeyekiuka kifungu 4:4 atakuwa ametenda kosa.Adhabu kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake**.

**4:5. KUBADILI MAJINA AU ANUANI**

(i). Endapo jina la mwanafunzi au anuani ya mzazi/ mlezi vitabadilika kwa sababu yoyote ile, taarifa ya kimaandishi itolewe shuleni ili rekodi ziwekwe sahihi.

(ii). Majina yaliyoandikishwa shuleni ndiyo yatakayotumika bila kubadilishwa.

(iii). Jina la mwanafunzi linaweza kubadilishwa endapo hati maalumu ya mahakama itaambatanishwa kwenye maombi ya kubadili jina.

**Mwanafunzi atakayebadilisha anuani, jina, au kutumia majina yasiyo maalumu (nick names) kama yanavyosomeka kwenye usajili, atakuwa ametenda kosa. Adhabu kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.**

**4:6 WAGENI**

(i). Wageni hawaruhusiwi kufika shuleni kuonana na mwanafunzi wakati wowote awapo shuleni. Iwapo kuna tatizo kubwa mfano kufiwa, taarifa zitolewe kwa Mkuu wa Shule. Utaratibu wa kumjulisha mwanafunzi utatolewa na Mkuu wa Shule.

(ii). Pale itakapolazimu, wazazi/walezi watapokelewa shuleni siku za kazi kuanzia saa tatu (2:00)Asubuhu hadi saa nane mchana.

(iii). Wageni wote wafike mapokezi /ofisi ya walimu kwanza kabla ya kumwona mwanafunzi.

(iv). Mwanafunzi haruhusiwi kuzungumza/kuonana na mgeni bila ruhusa.

(v). Wageni wataelekezwa eneo la kukaa. Ni marufuku kukaa na mgeni sehemu isiyo rasmi.

(vi). Wazazi/walezi hawaruhusiwi kufika shuleni siku za Jumamosi, Jumapili na sikukuu.

**Mwanafunzi yeyote ambaye Mzazi/Mlezi wake atakiuka kifungu 4.6 (i) – (v) atakuwa ametenda kosa. Adhabu itatolewa dhidi ya mwanafunzi.**

**5:0. MENGINEYO.**

**5.1** Ni jukumu la mzazi/mlezi kumpatia mwanafunzi fedha kwaajili ya matumizi binafsi awapo shuleni pamoja na kugharamia usafiri wa kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo.
Fedha hizi apewe mwanafunzi mkononi, mzazi akadirie vema matumizi ya mwanae ili asiwe mbadhirifu au mdokozi.

**5.2** Ni jukumu la mzazi/mlezi kuhakikisha afya bora ya mwanae kwa kumpatia matibabu stahiki kabla ya kuja shuleni. Mwanafunzi mwenye maradhi ya kudumu aje na barua ya uthibitisho kutoka kwa daktari wa hospitali ya Wilaya, Mkoa au Rufaa. Aidha mwanafunzi apatiwe fedha za matibabu kwa dharura itakayojitokeza.

**5.3** Mwanafunzi awe na vifaa vya usafi binafsi kama vile doti moja ya kitenge (asije na kanga),nguo za ndani,taulo za kike (Pads), taulo, mswaki, sabuni, mafuta ya kupakaa n.k(manukatoha yaruhusiwi)

**5.4** Ni mategemeo yangu makubwa kwamba Mwanafunzi atasoma kwa bidii, atatoa ushirikiano kwa Wenzake, kwa Walimu na Watumishi wengine na atazitii kanuni na sheria za shule katika kipindi chote awapo shuleni ili kuleta ufanisi na maendeleo ya shule.

**5.5** Kila mwanafunzi aandike jina lake katika sare zake zote za shule pamoja na vifaa vyake vyote binafsi ili kuepuka kuchangia ua kupotea

**5.6** Kabla ya kuripoti shuleni mwanafunzi ajaze fomu zifuatazo na aje nazo:

**5.6.1** Fomu ya taarifa ya Mwanafunzi na ya kukubali kujiunga na Shule.( Ijazwe na Mwanafunzi na kuthibitishwa na Mzazi)

**5.6.2** Fomu ya uchunguzi wa afya( Medical examination form)

**5.7**Mzazi/Mlezi: Mawasiliano yote yamhusuyo mwanao yafanyike kupitia namba za simu zilizo katika Fomu hii. Epuka mawasiliano na mtu mwingine asiejulikana ili usitapeliwe. Usitume pesa kwa Mtu yoyote atakayekupigia bila kupata uthibitisho toka Shuleni.

**5.7** Hatupokei wanafunzi siku za Jumamosi, Jumapili, sikukuu na usiku(kwa sababu za kiusalama)

**NB:SIMU, chaja ya simu, LAINI ya SIMU, PASI ya umeme na HEATER havitakiwi shuleni kamwe.**

6:0.Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA BUTUNDWE SEKONDARI**

**"Elimu kwa Huduma"**

..............

**MWL. HAPPINESS ADONIAS MANYAMA**

**(MKUU WA SHULE)**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI BUTUNDWE
S.L.P. 442
GEITA

**SHULE YA SEKONDARI BUTUNDWE ORODHA YA VITABU KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO.**

Kwa sababu mwanafunzi anakuja shuleni kwa lengo kuu la kusoma, shule imeazimia kuwataarifu wazazi/walezi ambao watoto wao wanajiunga na shule nii katika kidato cha tano kuwanunulia vitabu kulingana na Tahasusi(combination) zao. Ifuatayo ni orodha ya vibatu vilivyopendekezwa,mzazi anaweza kununua idadi ya vitabu kulingana na uwezo wakekiuchumi. Hivi vitabu ni vya mwanafunzi mwenyewe.

**GENERAL STUDIES (GS)**

1. General studies notes -Nyambari Nyangwine.
2. General studies supplementary Book for A-level and Colleges,Civic Education Teachers Association(CETA)-2010.
3. JOANNNES BIGIRWAMUNGU (etalal)5thEdition 2019 UNDERSTANDING
4. Gereral studies for advanced leveL APE DSM.
5. Mbalase Book 1 & 2.
6. General studies for V & VI BY Mwaipaja M (2018)

**BASIC APPLIED MATHEMATICS( BAM)**

1. Pure and Applied Mathematics-C.J Tranter.
2. Adv math 1-C.W.Celia

**BIOLOGY.**

1. Biological science (BS) – D.J. Taylor, N.P.O Green, G.W, Stout.
2. New understanding Biology-P.O Green and Nelson Thomas
3. S. Chand class XI &XII

**CHEMISTRY.**

1. Understanding Chemistry for Advanced level
2. Chand – Volume I&II
3. A-Level Chemistry-E.N Ramsden (4th Edition)
4. Physical Chemistry- Mark Daniel.
5. Inorganic Chemistry- Mzumbe Books Project

**AGRICULTURE.**

1. Introduction to Agromechanics-Dr.H.O. Dihenga.
2. Soil Science-G.Lombin
3. Farm Mechanization- U.G.N.Anazodo
4. Weeds Science-I.O.Akobundu.
5. Animal Health- G.I.Onura